# MT. ANTONI WA PADUA

*Sala na Novena ya siku 9*



ANGELA BENEDICT KESSY

Scanned with CamScanner

# MTAKATIFU ANTHONY WA PADUA

## Padre na Mwalimu wa Kanisa

Mtakatifu Anthony alizaliwa Lisbon nchini Ureno mwaka 1195, na wazazi wa ukoo bora. Mama wa Anthony alimfundisha mtoto wake kutaja majina ya Yesu na Maria. Anthony alipopata umri wa miaka kumi na mitano aliingia katika Shirika la Mtakatifu Augustino wa Hippo. Hapo alifanya bidii katika masomo yake, akajifunza maarifa yote ya nyakati hizo.

Baada ya miaka tisa alipewa daraja la upadre, kisha alijiunga na Shirika la Wafransisko, akataka kwenda kuhubiri Injili kwa watu wa Afrika. Anthony alikuwa na mapendo makubwa sana kwa Bwana wetu Yesu Kristo na alitamani kufa kwa ajili yake. Basi, aliomba ruhusa kwa wakuu wake aende Afrika ili awe mfiadini; wakakubali. Alipokuwa njiani kuja Afrika alipatwa na homa kali, na hivi badala ya kwenda Afrika ilimbidi arudi. Merikebu yake iliyumbishwa huko na huko na mawimbi ya bahari mpaka kisiwa cha Sisilia karibu na Italia.

Alipofika huko katika nyumba ya Wafransisko, mara ya kwanza hawakumtambua Anthony kwamba ni mtoto wa jamaa bora, na mtu mwenye akili na



Scanned with CamScanner

utakatifu. Padre mkuu alimtuma kwenda kuosha vyombo vya mezani. Lakini, siku moja alipoambiwa na Padre mkuu afundishe kanisani, akafundisha vizuri sana. Watu waliohudhuria kanisani walipigwa na bumbuazi. Ndipo Padre mkuu wa monasteri alimwondoa jikoni alikokuwa akiosha sahani za mezani. Alimfanya kuwa mwalimu wa wanafunzi wa shirika, akapewa kazi ya kuwafundisha watu dini.

Mt. Antony amewahi kuandika kwamba, wakristo ni lazima watabasamu na kufurahi pamoja na Bikira Maria kwa kumwilishwa kwake Kristo Yesu kwa ajili ya wanadamu, lakini pia ni lazima kushiriki mateso yake kama alivyoshiriki Bikira Maria akimuona mwanae akiuawa msalabani. Ni katika kushiriki yote hayo ambapo Mama huyu alibaki kuwa mwaminifu mpaka mwisho, ndio sababu mwanae alipenda kumpaliza mbinguni.

Mt. Anthony alifariki alipokuwa na umri wa miaka thelathini na sita, mjini Padua (Italia) mwaka 1231. Mwaka mmoja baada ya kifo chake, mnamo mwaka 1232, aliandikwa katika orodha ya watakatifu, na mwaka 1946 Papa alimtaja kuwa Mwalimu wa Kanisa.

***MTAKATIFU ANTHONY WA PADUA, UTUOMBEE.***



Scanned with CamScanner

## SALA YA KILA SIKU KWA MT. ANTHONY WA PADUA

Ninakusalimu wewe uliye Mkuu Mt. Anthony wa Padua na kufurahia juu ya mapaji ambayo Bwana wetu ameamua kuyaweka kwako. Ninakukumbusha hasa pale mtoto Yesu aliposhuka ukamshike mikononi na kukulinda. Oh! Nifuraha iliooje iliojaa moyo wako muda huo. Kwa bahati hii iliyo kuu na kwa maono yenye heri ambapo kwa sasa unamuona uso kwa uso, ninakuomba na ninakusihi Mt. Anthony, unisaidie mimi katika matatizo yangu, hofu zangu hasa katika hili **(taja shida yako)**. Oh! Ninakuomba moyo wako uguswe kuniombea mimi usikie na kunijibu. Mwambie Bwana wetu Yesu Kristo juu ya mahitaji yangu mimi ninayesali kupitia maombezi yako. Neno moja, alama moja, ambayo Yesu aliipenda ndani ya moyo wako itafanya nipate mahitaji yangu na kunifanya nijawe furaha na shukrani. Amina.

**Baba yetu, Salamu Maria na Atukuzwe Baba.**

**K.** Utuombee Mt. Anthony

**W.** Tupate kustahilishwa ahadi za Kristo.



Scanned with CamScanner

## SALA KUOMBA MSAADA KWA ROHO MTAKATIFU

Umtume Roho Mtakatifu ndani ya moyo wangu ili niweze kuelewa, katika akili yangu ili niweze kukumbuka, na katika roho yangu ili niweze kutafakari. Nivuvie mimi niweze kuongea kitakatifu, kiukarimu, na kwa huruma. Nifundishe na ongoza mawazo yangu na milango yangu ya fahamu mwanzo mpaka mwisho. Ninakuomba neema yako iniongoze na kunirekebisha daima ninakuomba sasa niongozwe na hekima kutoka juu kwasababu ya huruma yako ya daima. Amina.

## SALA YA KUMWOMBA MT. ANTHONY WA PADUA KATIKA JAMBO GUMU

Mtukufu Mt. Anthony, rafiki yangu na mlinzi wangu, ninakuja kwako kwa ujasiri katika shida yangu. Katika miminiko la ukarimu wako unawasikia wote wanaokuja kwako. Umaarufu wako katika kwenda katika kiti cha enzi ni wa pekee kiasi kwamba Mungu anakujalia kila uombalo. Tafadhali pokea ombi langu nyoofu licha ya kutokustahili kwangu na dhambi zangu. Ninakuomba utazame tu upendo wa daima wa Yesu na Maria na tamaa yangu ya utukufu wao na huruma. Ninakuomba uniombee neema ninazo hitaji kadiri ya mapenzi ya Mungu na kwa manufaa ya roho yangu. Ninakabidhi kwako ombi hili kwa njia ya mtoto Yesu. Nibariki mimi mbarikiwa Mt. Anthony kwa Jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu. Amina



Scanned with CamScanner

## SALA YA KUTAFUTA KITU KILICHOPOTEA MT. ANTHONY WA PADUA

Ee Mtakatifu Anthony wa Padua,/ uliye mpole kati ya watakatifu wote./ Upendo wako kwa Mungu na kwa binadamu/ wakati ulipoishi hapa duniani,/ umetustahilia uwezo wa kutenda miujiza mingi/ kwa ajili ya wale wenye shida./ Kwa hiyo sisi pia/ tunapata moyo wa kukimbilia kwako/ na kuomba msaada wako. Labda ombi letu haliwezi kutimizwa bila muujiza!/ Hata hivyo huitwi Mtakatifu wa miujiza?/ Kwa hiyo Mtakatifu Anthony wa Padua mwenye upole/ na huruma sana kwa watu wenye shida,/ sikiliza maombi yetu/ na kuyapeleka mbele ya Mtoto Yesu/ aliyependa kukaa mikononi mwako./ Nasi tutakuonesha shukrani kubwa katika maisha yetu yote. **/ Amina.**

## SALA YA MWANAFUNZI (MT. ANTHONY WA PADUA)

Mtakatifu Anthony wa Padua, ninaweka masomo yangu chini ya ulinzi wako wenye nguvu. Kwa njia ya maombezi yako, kupitia Roho Mtakatifu nijalie mwanga, nguvu, akili na unyenyekevu ili niweze kujua yale yote ninayofundishwa na ninayojifunza. Ninakusihi Muumba wa mbingu na vitu vyote unipe uwezo wa kufahamu mambo kwa usahihi, na vipaji halisi katika maelezo yangu. Amina.



Scanned with CamScanner

# NOVENA KWA MT. ANTHONY WA PADUA

## SIKU YA KWANZA

Ee Mtakatifu Anthon, mnyenyekevu katika watakatifu,upendo wako kwa Mungu na ukarimu kwa viumbe vyake umekufanya kustahilishwa ukiwa duniani kupokea nguvu ya miujiza. Miujiza ilisubiri neno lako, ambalo daima ulikuwa tayari kuliongea kwa wale waliokuwa katika hofu na matatizo. Kwa kutiwa moyo na wazo hili ninakuomba uweze kupatiwa hitaji ninaloomba katika novena hii **(taja hitaji lako).** Jibu la ombi langu huenda likahitaji muujiza, hata hivyo wewe ni mtakatifu wa miujiza. Ee Mtakatifu na mnyenyekevu Mt. Anthony, ambapo daima moyo wako ulikuwa umejawa na huzuni ya kibinadamu, ninakuomba umnong'oneze mtoto Yesu ombi langu katika sikio, ambaye daima alikubali kupokelewa katika mikono yako na shukrani ya moyo wangu itakuwa daima juu yako.

**Baba yetu, Salamu Maria na Atukuzwe Baba**

Mt. Anthony wa Padua utuombee.



Scanned with CamScanner

## SIKU YA PILI

Ee Mtakatifu mtenda miujiza Anthony wa Padua kumbuka haijawahi kuwa ngumu kumuacha mtu anayekimbilia kwako kuomba msaada wa maombi yako. Nikiwa na ujasiri huo ninakuomba sasa, tena nikiwa naamini kabisa sitakataliwa, ninaruka kabisa kuomba ulinzi kwako, wewe ambaye ni mpendwa wa mtoto Yesu. Ee tajiri mwaminifu wa huruma ya Mungu, ninakuomba usiliache ombi langu bali ninakuomba uyapeleke kwenye kiti cha utukufu cha Mungu, ukiyapa nguvu kwa maombezi yako ili niweze kupata yale mahitaji ninayo omba katika novena hii **(taja hitaji lako)**.

**Baba yetu, Salamu Maria na Atukuzwe Baba**

Mt. Anthony wa Padua utuombee.

## SIKU YA TATU

Ee msafi sana Mt. Anthony, wewe ambaye kwa njia ya fadhila za kimalaika ulijaliwa kumbeba mtoto Yesu katika mikono yako na kumuweka karibu na moyo wako. Ninakuomba unikinge na ubaya wowote uliopangwa kwa ajili yangu. Ee Mt. Anthony uliyezaliwa chini ya ulinzi wa Maria Imakulata, katika sikukuu ya kupalizwa kwake



Scanned with CamScanner

Mbinguni, ambaye ulijitoa kwake na sasa ni mwombezi mwenye nguvu huko mbinguni, ninakuomba unipatie hitaji ninalokuomba katika novena hii **(taja hitaji lako)**. Ee mkuu wakushangaza na mtendaji niombee kwa Mungu niweze kujaliwa hitaji langu.

**Baba yetu, Salamu Maria na Atukuzwe Baba**

Mt. Antony wa Padua utuombee

**SIKU YA NNE**

Ninakusalimu na kukuheshimu, Mt. Anthony. Ulimwengu wa wakristo unageukia kwako na kupata huruma yako na nguvu ya msaada katika mahitaji yao na katika mateso yao ninaomba uniombee faraja katika kupata jibu kwa mahitaji yangu ninayo omba katika novena hii **(taja hitaji lako)** Ee Mtakatifu Anthony, ninakuomba unisaidie kupata neema ninazo ziomba.

**Baba yetu, Salamu Maria na Atukuzwe Baba**

Mt. Antony wa Padua utuombee

Scanned with CamScanner

## SIKU YA TANO

Ninakusalimu Mt. Anthony ua la Utakatifu, manukato na utukufu katika ukristo. Ninakusalimu Mtakatifu mkuu, kerubi wa hekima na serafi wa upendo ya Kimungu. Ninazifurahia karama alizokupa Mungu. Kwa unyenyekevu na ujasiri ninajiweka katika msaada wako, kwani nina amini Mungu amekupatia pia ukarimu, huruma na nguvu. Ninakuomba kwa upendo uliouhisi kutoka kwa Mtoto Yesu ulipomshika kwa mikono yako, ninakuomba umwambie hitaji langu **(taja hitaji lako)**

**Baba yetu, Salamu Maria na Atukuzwe Baba**

Mt. Anthony utuombee

## SIKU YA SITA

Ee mtukufu Mt. Anthony, uliyechaguliwa na Mungu kuhubiri neno lake, ulipokea kutoka kwake karama ya ndimi na nguvu ya ajabu ya kutenda miujiza. Ee Mt. Anthony niombee ili niweze kutimiza mapenzi ya Mungu katika kila kitu ili niweze kumpenda yeye na wewe milele yote. Ee Mt. Anthony, ninakuomba unisaidie kupata neema ili niweze kupata hitaji ninaloomba katika novena hii **(taja hitaji lako)**

**Baba yetu, Salamu Maria na Atukuzwe Baba**

Mt. Antony wa Padua utuombee



Scanned with CamScanner

## SIKU YA SABA

Ee Mshindi wa imani ya Kristo, Mt. Anthony, Mtukufu katika miujiza yako mingi, ninakuomba unipatie mimi hazina ya Bwana wetu na Mungu wetu neema ninayo hitaji hasa katika novena hii **(taja ombi lako)**. Ee Mt. Anthon msikivu daima kwa wale waliokualika, nijalie msaada wa maombi yako.

**Baba yetu, Salamu Maria na Atukuzwe Baba**

Mt. Antony wa Padua utuombee

## SIKU YA NANE

Ee Mtakatifu, Mt. Antony, umejionesha mwenyewe kuwa mwenye nguvu katika maombi yako, wewe ni mnyoofu na mkarimu kwa wale wote wanaokuheshimu na kukuomba wewe, katika shida na machungu. Ninakuomba wewe uliye mnyenyekevu, uniweke mimi daima chini ya ulinzi wako katika hitaji langu la sasa ili niweze kulipata **(taja hitaji lako)**. Ninakuomba upeleke ombi langu kwa malkia wa Mbingu, ili aweze kuniombea hitaji langu pamoja nawe mbele ya kiti cha huruma ya Mwanae Yesu Kristo.

**Baba yetu, Salamu Maria na Atukuzwe Baba**

Mt. Antony wa Padua utuombee



Scanned with CamScanner

## SIKU YA TISA

Mt. Anthony mtumishi wa Mama Maria, utukufu wa kanisa, muombee Baba Mtakatifu, Maaskofu wetu, Mapadre wetu, waseminari na mashirika yetu ya kitawa, ili kwa njia ya tamaa yao ya utakatifu na kazi zao njema wote waungane katika imani na kumpa Mungu utukufu mkuu. Mt. Anthony msaada wa wale wanaokuomba, sali nami na niombee mbele ya kiti cha Mungu Mwenyezi ili niweze kupata hitaji ninalo liomba katika novena hii **(taja ombi lako)**

**Baba yetu, Salamu Maria na Atukuzwe Baba**

Mt. Antony wa Padua utuombee

Tunaomba huruma ya Mungu ibaki nasi daima.

Roho za waamini marehemu wapate rehema kwa Mungu wapumzike kwa amani. Amina.

Ee Mungu, tunapomkumbuka Mt. Anthony wa Padua, Muungamishi, tunaomba iwe ni sababu ya furaha katika kanisa lako, liweze kukuzwa daima na msaada wake na liweze kustahilishwa kupata furaha ya milele. Kwa njia ya Kristo Bwana wetu. Amina



Scanned with CamScanner

# LITANIA YA MT. ANTHONY WA PADUA

*(sali binafsi tuu)*

Bwana utuhurumie — Bwana utuhurumie
Kristo utuhurumie — Bwana utuhurumie
Bwana utuhurumie — Bwana utuhurumie
Kristo utusikie — Kristo utusikilize
Baba wa mbinguni Mungu, ................ utuhurumie
Roho Mtakatifu Mungu, ..................... utuombee
Utatu Mtakatifu Mungu mmoja............ utuhurumie
Maria Mtakatifu ..................................... utuombee
Mt. Anthony wa Padua.......................... "
Mt. Anthony utukufu wa ndugu wadogo "
Mt. Anthony nguzo ya wosia wa Mt. Fransisko
Mt. Anthony hekalu la hekima ya Mbinguni "
Mt.Anthony mharibu wa ubatili wa dunia "
Mt. Anthony aliyeshinda katika utakatifu "
Mt. Anthony mfano wa unyenyekevu..... "
Mt. Anthony mpenda msalaba .............. "
Mt. Anthony mfiadini wa tamaa............. "
Mt. Anthony aliyejawa ukarimu ............ "
Mt. Anthony mpenda haki .................... "
Mt. Anthony tishio kwa wasiomwamini Kristo "
Mt. Anthony mfano wa ukamilifu........... "
Mt. Anthony mfariji wa wanaoteseka ..... "
Mt. Anthony mrudisha vilivyopotea........ "
Mt. Anthony mlindaji wa wale walioonewa "
Mt. Anthony mfungua wafungwa .......... "
Mt. Anthony muongoza wahujaji........... "
Mt. Anthony mrudisha afya ................. "



Scanned with CamScanner

Mt. Anthony mtenda miujiza .................. "
Mt. Anthony mrudisha sauti iliyopotea... "
Mt. Anthony mfungua viziwi .................. "
Mt. Anthony mfukuzaji wa shetani ......... "
Mt. Anthony mrudisha uhai .................. "
Mt. Anthony mfukuza hofu .................. "
Kutoka katika mitego ya shetani...
**Utuopoe Ee Mt. Anthony**

Kutoka katika radi na mafuriko
**Utuopoe Ee Mt. Anthony**

Kutoka katika maovu ya roho na mwili
**Utuopoe Ee Mt. Anthony**

Kwa njia ya maombi yako **Utuopoe Ee Mt. Anthony**
Katika maisha yetu yote, **Mt. Anthony utulinde**
Mwanakondoo wa Mungu, unayeondoa dhambi za dunia **Utusamehe Ee Bwana.**
Mwanakondoo wa Mungu uondoae dhambi za dunia **Utuhurumie Ee Bwana.**
Mwanakondoo wa Mungu uondoae dhambi za dunia **Utusikilize Bwana.**
Mt. Anthony utuombee tupate kujaliwa ahadi za Kristo.

**Tuombee.**

Ee Mungu,ninakuomba kwa njia ya Mt. Anthony wa Padua, muungamishi na mlinzi, ulipe kanisa furaha, ili liweze daima kuimarishwa kwa njia ya maisha yake ili liweze kupata tuzo la milele. Kwa njia ya Kristo Bwana wetu. Amina.



Scanned with CamScanner

## SALA YA KUOMBA ULINZI WA MAMA BIKIRA MARIA

Mama wa Mungu/Bikira Maria unikubali ninapokujia/ Mimi ni wako/nikiwa mzima Mimi ni wako nikizimia. Mimi ni wako katika mateso Mimi ni wako katika misiba. Mimi ni wako uwapo msalaba. Mimi ni wako kwa sasa na daima. Mama wa mungu Bikira Maria unikubali ninapokujia. Mama ninakutumainia/ nakutegemea. Mama nakung'ang'ania/nakulalamikia. Mama mwenye huruma/unisimamie. Mama mwenye uwezo /unihurumie. Uje Mama/unisaidie kusali. Uje Mama/unisaidie vitani. Uje Mama/ unisaidie taabani. Uje Mama/kaa nami kila mahali Unaweza kunisaidia / wewe mwezaji. Unapenda kunisaidia/mwenye upole Yakupasa kunisaidia/mwenye huruma. Mama wa neema/msaada wa wakristo. Makimbilio ya wakosefu. Mlango tunamotafutia wokovu; Matumaini yetu duniani. Pambo la mbingu/na la watakatifu.Wewe ni Tuzo la wenye uchungu. Nani amekuomba/ asipate msaada wako? Lini umedharau/sala za watoto wako. Nazidi kulia/ katika mateso na taabu: Daima Maria/ aleta misaada ya ajabu. Katika misiba /nikiwa kufani/nalia Daima po pote/ Ee Mama Maria saidia. Ninayo imani / na matumaini moyoni. Maria anipa / furaha za mbingu mwishoni. Mama wa Mungu /Bikira Maria. Unikubali ninapokujia./ Mimi ni wako / nikiwa Mzima Mimi ni wako/nikishazimia. Mimi ni wako/ katika mateso. Mimi ni wako/katika misiba. Mimi ni wako/ uwapo msalaba. Mimi ni wako/ kwa sasa na daima. Mama wa Mungu/ Bikira Maria Unikubali ninapokujia.

*********

**Salam Mariax1, Atukuzwe Babax1**



Scanned with CamScanner